ISO 21001:2018 CERTIFIED

TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM (DIT)

MAHAFALI YA ISHIRINI (20) YA TAASISI

Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) anawatangazia wahitimu na wadau wote wa DIT kuwa Mahafali ya Ishirini (20) duru ya kwanza Kampasi ya Kuu, Dar es Salaam yamepangwa kufanyika Ijumaa, tarehe **4 Desemba, 2026.** Duru ya pili Kampasi ya Mwanza yatafanyika tarehe **11 Desemba, 2026** na Duru ya tatu Kampasi ya Songwe yatafanyika tarehe **7 Januari, 2027.**

Mahafali ya Duru ya kwanza yatatanguliwa na siku ya utoaji tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao katika mwaka wa masomo 2025/2026, sherehe ambazo zitafanyika Jumatano, tarehe **2 Desemba, 2026.**

Taasisi inapenda kuwataarifu wahitimu wa Shahada ya Uzamili (M.Eng), Shahada ya Kwanza (B.Eng/B.Tech) na Stashahada ya Uhandisi na Teknolojia (OD) kusoma utaratibu na hatimaye kuthibitisha ushiriki wao katika Mahafali hayo kupitia tovuti ya Taasisi (www.dit.ac.tz).

Wahitimu watakaoshiriki wanapaswa kulipia joho la Mahafali Tshs. 30,000/= (kwa Wahitimu wa Stashahada za Uhandisi na Teknolojia (OD) na wale wa Shahada za kwanza za Uhandisi na Teknolojia, na Tsh 50,000/= (kwa wahitimu wa Shahada ya Uzamili). **Malipo hayo yafanyike kwa kutumia control number ambazo zinapatikana kupitia akaunti ya mwanafunzi ya SOMA.** *Watakaoruhusiwa kushiriki Mahafali haya ni wale tu watakaokamilisha malipo husika*.

ZINGATIA: Malipo yafanyike kwa kutumia jina kamili kama linavyoonekana kwenye orodha ya wahitimu wa mwaka 2025/2026 iliyopo kwenye tovuti ya Taasisi, namba ya usajili na madhumuni ya malipo yaani Mahafali.

"Rehersal" itafanyika Alhamis, tarehe **3 Desemba, 2026 - Saa 8** Kamili Mchana katika Ukumbi wa Diamond Jubilee - Upanga**.**

Mwisho wa kuthibitisha ushiriki na kulipia ni tarehe **30 Novemba, 2026.** Hakutakuwa na muda wa nyongeza baada ya tarehe hii.

Tangazo hili limetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano na Masoko,
Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam,
S.L.P 2958,
Dar es Salaam.